JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA
SHULE YA SEKONDARI LAMADI

SHULE YA SEKONDARI LAMADI
S.L.P 402,
BUSEGA.
Barua pepe: lamadisecondary@gmail.com
Simu: 0787-353080/0737-563023

Tarehe:.....

Kumb.Na.LSS/AD/VOL...../.....

JINA LA MWANAFUNZI:.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LAMADI ILIYOKO WILAYA YA BUSEGA NKOA WA SIMIYU MWAKA 2021.

01. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **LAMADI** iliyopo umbali wa **KM 1** kutoka mji mdogo wa Lamadi na ipo katika kitongoji cha **MWALUKONGE.**

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11-01-2021.** Hivyo, unatakiwa kuripoti shuleni bila kuchelewa kuanzia tarehe **11-01-2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25-01-2021** na usiporipoti ndani ya muda husika, nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine.

02. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(a) SARE YA SHULE

(i) WAVULANA

- Suruali ya dark blue **(bluu iliyokolezwa)** yenye malinda mawili na isiwe ya kubana **(modo).**
- Shati nyeupe ya mikono mifupi.
- Soksi nyeupe ndefu.
- Mkanda mweusi usio na urembo.
- Viatu vyeusi vya kuchomeka visivyo na kamba.

(ii) WASICHANA

- Sketi ya dark blue **(bluu iliyokolezwa)** ndefu mpaka kwenye miguu, yenye marinda makubwa ya inchi nne.
- Shati nyeupe ya mikono mifupi.
- Soksi nyeupe ndefu.
- Viatu vyeusi vya kuchomeka visivyo na kamba **(simple).**
- Rangi ya hijabu **(kwa waislam)** ifanane na sare ya shule hii **(nyeupe).**

(b) SARE YA MICHEZO

- Trakisuti ya dark blue **(bluu iliyokozwa).**
- Raba za michezo
- T-sheti ya dark blue **(bluu iliyokozwa).**

(c) MAHITAJI MENGINE

- Daftari **(counter books)** kumi, kalamu na mkebe wa hesabu.
- Kila mwanafunzi aje na ufagio wa chelewa kwa ajili ya kusafishia mazingira ya shule.

03. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa **sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **sheria Na.10 ya mwaka 1995.** Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini.

Hivyo, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la msingi.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni **LAZIMA.**
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio jioni **(preparation).**
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili wako, mavazi na mazingira ya shule ni **LAZIMA.**
(g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapokuwa shuleni ni **LAZIMA.**
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutunza mali za umma.

04. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE.

(a) Wizi.
(b) Uasherati na ushoga.
(c) Ubakaji.
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile **bangi, cocaine, mirungi, kubeli, n.k**
(e) Kupiga au kupigana.
(f) Kuoa au kuolewa.
(g) Kumiliki/kuwa na simu ya mkononi.
(h) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(i) Kudharau Bendera ya Taifa pamoja na Wimbo wa Taifa.
(j) Kuwa mjamzito/kupata mimba pia kusababisha mimba au ujauzito.
(k) Kutoa mimba.
(l) Kugoma, kuchochea au kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(m) Kukataa adhabu kwa makusudi.

05. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

(a) **Medical Examination Form** ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni **(KIAMBATANISHO B)**
(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai na mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule **(KIAMBATANISHO A)**

NB: Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
JOHN MOSSES MAGOLANGA
MKUU WA SHULE

‘KIAMBATANISHO A’

FOMU YA MKATABA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LAMADI

(Anwani ya mzazi/mlezi)
.....
.....
.....
Tarehe.....

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI LAMADI,
S.L.P 402,
BUSEGA.

SEHEMU ‘A’ IJAZWE NA MWANAFUNZI

Mimi.....ambaye ni mvulana/msichana niliyekuwa nasoma shule ya msingi .....Wilaya ya Busega, Mkoa wa Simiyu. Nakubali kujiunga na Shule ya Sekondari Lamadi iliyopo Wilaya ya Busega, Mkoa wa Simiyu leo tarehe..... **Nitazingatia na kutii sheria za shule hii.** Nitakuwa mwaminifu, Mwenye bidii na juhudi katika masomo, kazi za nje na michezo.

JINA LANGU.....SAINI.....

TAREHE.....

SEHEMU ‘B’ IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

Mimi.....Mzazi/mlezi wa.....

Ninayeishi kitongoji cha .....kijiji cha.....Wilaya ya Busega, Mkoa wa Simiyu. Nakubali mtoto wangu kujiunga na kusoma katika Shule ya Sekondari kuanzia Tarehe.....hadi atakapohitimu kidato cha Nne. Mtoto wangu nitampatia mahitaji yote yanayotakiwa Shuleni. Nitahakikisha ninafuatiliakwa ukaribu sana Mahudhurio, mwenendo na maendeleo yake shuleni.hivyo, sitasita kumuonya na kuchukua hatua za kisheria pale anapobainika kutenda kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu za Shule.

JINA LANGU.....SAINI.....

TAREHE.....

‘KIAMBATANISHO B’

APPLICATION FORM FOR MEDICAL EXAMINATION
LAMADI SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 402 BUSEGA

To be completed by a medical officer in request of all FORM 1 ENTRANTS.

Full name:.....

Age:..... sex.....

Stool Examination.....

Blood count (Red and White).....

Urine analysis.....

Syphilis test.....

T.B test .....

Eye test.....

Ear.....

Chest.....

Spleen.....

Pregnancy test.....Gestation.....(for girls)

ADDITION INFORMATION: (e.g, Physical defects or impairment(s) infections or chronic diseases requiring special treatment)
.....
.....
.....
.....

I certify that I have examined the above student and recommend that he/she is **fit/unfit** to pursue further education.
Name:.....
Signature:.....
Designation:.....
Station.....
Date.....
(Nb: At a time of examination, please treat the individuals for any ailment you noted)